Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADALIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KWANZA

**Kikao Cha Kwanza - Tarehe 28 Desemba, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Kumi na Moja Jioni)*

## TANGAZO LA RAIS LA KUITISHA MKUTANO WA BUNGE

**ND. DAMIAN S. L. FOKA – KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie. Naomba tuendelee na shughuli. Naomba kupata nafasi ya kusoma tangazo la Rais, la kuitisha Mkutano huu. Tangazo la Rais, la kuitisha Mkutano wa Bunge, limetolewa chini ya Ibara ya 90 (1) ya Katiba ya Nchi.

"Kwa kuwa kwa mujibu wa Ibara ya 90 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Rais anatakiwa kuitisha Mkutano wa Bunge jipya, ufanyike kabla ya kupita siku saba tangu kutangazwa kwa matokeo ya Uchaguzi Mkuu katika Majimbo ya Uchaguzi yote isipokuwa katika Majimbo yale ambapo uchaguzi umefutwa na kufanywa upya na kwa kuwa matokeo ya Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 14 Desemba, 2005 sasa umekwisha kutangazwa. Kwa hiyo basi, mimi Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sasa ninauitisha Mkutano wa Bunge jipya ufanyike Dodoma, tarehe 28/12/2005 kuanzia saa 11:00 Jioni. Kwa kuthibitisha hati hii, ninaweka sahihi yangu na kuiwekea hati na muhuri wa Jamhuri ya Muungano leo tarehe 22 Desemba, 2005."

Ndio siku Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ameweka sahihi katika hati hii. Mwisho wa tangazo. *(Makofi)*

Baada ya uhalali wa kuitisha Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge, naomba sasa tusimame ili tusome dua.

*(Hapa Wabunge Wote Walisimama kwa ajili ya Dua)*

## D U A

*Katibu wa Bunge (Ndg. Damian S. L. Foka) Alisoma Dua*

## UCHAGUZI WA SPIKA

**KATIBU WA BUNGE:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa Bunge letu hili kama mnavyoona halina Spika, kazi ya kwanza itakayotekelezwa nanyi Waheshimiwa Wabunge hivi punde ni kumchagua Spika.

Kabla hamjatekeleza jukumu hili, hatuna budi kwanza apatikane Mwenyekiti, atakayetuongozea shughuli hizi. Jambo hili linatekelezwa kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni (3) ya Kanuni ya 19 ya Kanuni za Bunge ambayo inasomeka kama ifuatavyo:-

"Mara baada ya Dua kusomwa, Bunge litaingia katika shughuli ya kuchagua Spika. Kwanza, Katibu wa Bunge atamwomba Mbunge asiyekuwa Waziri awe mgombea wa nafasi hiyo ya Spika, kutoka miongoni mwa Wabunge ambao wamekuwa Wabunge kwa mfululizo kwa muda mrefu zaidi kuliko Wabunge wengine awe Mwenyekiti wa Bunge kwa madhumuni ya kuongoza shughuli za uchaguzi wa Spika, kisha atagawa karatasi za kura kwa Wabunge na uchaguzi wa Spika utafanywa kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa na Kanuni ya saba." Mwisho wa kunukuu.

Kumbukumbu zetu zinaonyesha kuwa, Mbunge mwenye sifa zinazotajwa na Kanuni niliyoinukuu ni Mheshimiwa Anne Semamba Makinda. Ni Mbunge wa Njombe Kusini.

Aidha, kumbukumbu hizo zinatiliwa uzito mkubwa wa suala zima la *gender sensitivity.* Hivyo basi, ninamwomba Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, aje akalie Kiti hiki cha Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

*Hapa (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kutoa maelezo. Kwa mujibu ya Ibara ya 86 ya Katiba ya Nchi ambayo inasomeka kama ifuatavyo:- Kutakuwa na Uchaguzi wa Spika, katika Mkutano wa Bunge jipya na katika Kikao cha kwanza chochote, mara baada ya kutokea nafasi katika Kiti cha Spika.

Mimi kama Msimamizi wa Uchaguzi wa Spika, nilitoa matangazo kwenye gazeti la Serikali namba 704 na 705 yote ya tarehe 11/11/2005 kueleza kuhusu uwazi wa Kiti cha Spika na uchaguzi wake kwa lengo la kuwafahamisha kuwa wale wote wenye sifa waniletee maombi yao ikiwa ni pamoja na kufuata masharti yaliyoko kwenye kifungu cha 38 cha sheria ya uchaguzi ya mwaka 1985 hadi tarehe ya mwisho, yaani siku ya leo nimepokea maombi ya mtu mmoja tu naye ni Mheshimiwa Samwel John Sitta. *(Makofi)*

Huyo kwa mujibu ya masharti ndio pekee aliyeweza kufanya hivyo na kama tulivyoelezana asubuhi kwa mujibu wa kifungu cha saba cha Kanuni, tumeelezana kwamba kama atakuwa ni mgombea mmoja, basi huyo atakuwa amechaguliwa bila ya kupingwa. Naomba niisome tena. "Endapo hadi kufikia saa 10 jioni ya siku ya uteuzi kutakuwa na jina moja tu lililokwishawasilishwa kwa msimamizi wa uchaguzi, basi

mgombea huyo atatangazwa na msimamizi wa uchaguzi kuwa amechaguliwa bila kupigwa kuwa Spika. *(Makofi)*

Kwa ajili hiyo, napenda kumtangaza Ndugu Samweli John Sitta kuwa ndio amepita bila kupigwa na nilikuwa naomba sasa Mwenyekiti, awateue watu wa kuweza kumwita popote pale alipo wamtafute aje hapa ili aape.

**MHE. ANNE. S. MAKINDA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kuwapongezeni wote ambao mmechaguliwa na wananchi kuingia katika Bunge hili na wale walioteuliwa na Mheshimiwa Rais na wale Wabunge ambao wamepitia Viti maalum, wote naomba niwapongeze sana. *(Makofi)*

## KIAPO CHA SPIKA

**KATIBU WA BUNGE:** Kiapo cha Spika.

**KATIBU WA BUNGE:** Ahsante sana.

*(Hapa Mheshimiwa Samweli J. Sitta aliapa na kukalia Kiti cha Uspika ndani ya Ukumbi wa Bunge)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikukabidhi Kanuni za Bunge pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakukaribisha uchukue Kiti chako, karibu. *(Makofi)*

**WABUNGE:** Joho! Joho!

## SHUKRANI ZA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msiwe na papara.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni nitatumia muda mfupi sana kutimiza wajibu muhimu sana na ninautimiza kwa furaha, wajibu huo ni kuwashukuru ninyi nyote kwa imani kubwa mliyoionyesha kwangu kunichagua kwa kauli moja kuwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010. (Makofi)

Nawashukuru sana na mzigo huu ni mkubwa sina uzoefu mkubwa sana kwa sehemu hii, haswa hii! Lakini nadhani kwa msaada wenu na ushirikiano wenu ambao nitautegemea wakati wote sina shaka upande wa Chama tawala na pia upande wa ndugu zetu upande wa upinzani tutaungana mkono ili tuisaidie Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iweze kutimiza majukumu yake kwa wananchi, majukumu ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa wale wanaotoka Mkoa wa Kilimanjaro watakumbuka kwamba nilipokuwa nao kule miaka ya nyuma nilitafsiri jina langu Samwel Sitta kwamba ni *Standards and Speed. (Kicheko/Makofi)*

Rais wetu wa awamu ya nne anazungumzia ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Mimi ni Spika wa *Standards and Speed*. Kwa hiyo, tutapenda tuliendeshe Bunge hili kwa kiwango cha juu sana cha ufanisi na mambo yaende haraka. Wale ndugu zangu ambao watachaguliwa katika Baraza la Mawaziri napenda niwatahadharishe kwamba majibu yasiyotoa ufumbuzi kwa matatizo halisi ya wananchi, Bunge hili nitaomba mniunge mkono tusiwe na uvumilifu na majibu ambayo yanafanya mzaha mbele ya shida halisi za wananchi wetu. *(Makofi)*

Baada ya utangulizi huo, kwa mujibu wa kanuni, mimi sijakamilika. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge kwa muda mfupi sana ili nirudi nikiwa rasmi na tuendelee na shughuli tulizozipanga. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa Bunge lilifungwa kwa muda kumpa nafasi Spika avae Joho Rasmi la Spika)*

*(Hapa Bunge lilirudia baada ya Spika kuwa Rasmi)*

**SPIKA:** Katibu endelea kutusomea shughuli za leo.

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, *agenda* inayofuata ni kiapo cha uaminifu kwa Waheshimiwa Wabunge.

**KIAPO CHA UAMINIFU KWA WAHESHIMIWA WABUNGE**

Mheshimiwa Spika, tuliona kwamba asubuhi tulikuwa tumetangaza kwamba kiapo kitakuwa kwa alphabet lakini tungependa tuanze na wafuatao:-

Mhe. Johnson P. Mwanyika
Mhe. Anne S. Makinda
Mhe. Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro
Mhe. Kabuzi Faustine Rwilomba
Mhe. Anne Margareth Abdallah
Mhe. Maida Hamad Abdallah
Mhe. Mohamed Rished Abdallah
Mhe. Mohammed Abdi Abdulaziz
Mhe. Rostam Abdulrasul Aziz
Mhe. Idd Mohamed Azzan
Mhe. Bahati Ali Abeid
Mhe. Juma Jamaldin Akukweti
Mhe. Dr. Ali Tarab Ali
Mhe. Fatma Othman Ali
Mhe. Ali Haji Ali
Mhe. Khadija Salum Ali Qassmy

Mhe. Aziza Sleyum Ally
Mhe. Ali Salum Ahmed
Mhe. Kheri Khatib Ameir
Mhe. Ame Pandu Ame
Mhe. Ameir Ali Ameir
Mhe. Afri Said Amour
Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili
Mhe. John Samwel Malecela
Mhe. Faida Mohamed Bakar
Mhe. Abubakar Khamis Bakary
Mhe. Prof. Feethan Filipo Banyikwa
Mhe. Elizabeth Nkunda Batenga
Mhe. Joel Nkaya Bendera
Mhe. Gosbert Begumisa Blandes
Mhe. Felister Aloyce Bura
Mhe. Dr. Batilda Salha Burian
Mhe. Dr. Cyril August Chami
Mhe. Hazara Pindi Chana
Mhe. Ania Said Chaurembo
Mhe. Dr. Raphael Masunga Chegeni
Mhe. Andrew John Chenge
Mhe. Gideon Asimulike Cheyo
Mhe. John Momose Cheyo
Mhe. Hezekiah Ndahani Chibulunje
Mhe. Amina Chifupa Mpakanjia
Mhe. Mathias Meinrad Chikawe
Mhe. Capt. John Zefania Chiligati
Mhe. Diana Mkumbo Chilolo
Mhe. Samwel Mchele Chitalilo
Mhe. Christopher Kajoro Chiza
Mhe. Mohammed Amour Chombon
Mhe. Dr. Maua Abeid Daftari
Mhe. Dr. David Mathayo David
Mhe. Paschal Constantine Degera
Mhe. Hasnain Gulamabbas Dewji
Mhe. Mohammed Gulam Dewji
Mhe. Anthony Mwandu Diallo
Mhe. Meryce Mussa Emmanuel
Mhe. Bakari Shamis Faki
Mhe. Col. Saleh Ali Farrah
Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji
Mhe. Stephen Jones Galinoma
Mhe. Dr. Zainab Amir Gama
Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia
Mhe. Ali Juma Haji
Mhe. Dr. Haji Mwita Haji

Mhe. Zuleikha Yunus Haji
Mhe. Hemed Mohammed Hemed
Mhe. Maria Ibeshi Hewa
Mhe. Parmukh Singh Hoogan
Mhe. Balozi Seif Ali Idi
Mhe. Issa Kassim Issa
Mhe. Yahya Kassim Issa
Mhe. Athumani Said Janguo
Mhe. Asha Mshimba Jecha
Mhe. Mwadini Abbas Jecha
Mhe. Rajab Ahmad Juma
Mhe. Shoka Khamis Juma
Mhe. Riziki Omar Juma
Mhe. Luhahula Emanuel Jumanne
Mhe. Gaudensia Mugosi Kabaka
Mhe. Siraju Juma Kaboyonga
Mhe. Phares Kashemeza Kabuye
Mhe. Mgeni Jadi Kadika
Mhe. Balozi Hamis Sued Kagasheki
Mhe. Janet Bina Kahama
Mhe. Charles Muguta Kajege
Mhe. Dr. Diodorus Buberwa Kamala
Mhe. Prof. Juma Athuman Kapuya
Mhe. Nazir Mustafa Karamagi
Mhe. Teddy Louise Kasella-Bantu
Mhe. Mariam Reuben Kasembe
Mhe. Eustace Osler Katagira
Mhe. Dr. Shukuru Jumanne Kawambwa
Mhe. Vita Rashid Kawawa
Mhe. Gaudence Cassian Kayombo
Mhe. Charles Ndeanaruwa Keenja
Mhe. Yono Stanley Kevela
Mhe. Salim Abdallah Khalfan
Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa
Mhe. Mwajuma Hassan Khamis
Mhe Salim Hemed Khamis
Mhe. Vuai Abdallah Khamis
Mhe. Abdisalaam Issa Khatib
Mhe. Hasan Rajab Khatibu
Mhe. Muhammed Seif Khatib
Mhe. Dr. Abdallah Omar Kigoda
Mhe. Dr. Aisha Omar Kigoda
Mhe. Hassan Chande Kigwalilo
Mhe. Godwin Fuya Kimbita
Mhe. Felix Mtibenda Kijiko
Mhe. Estherina Julio Kilasi

Mhe. Juma Hassan Killimbah
Mhe. Aloyce Bent Kimaro
Mhe. Halima Omari Kimbau
Mhe. Paul Peter Kimiti
Mhe. Rosemary Kasimbi Kirigini
Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga
Mhe. Grace Sindato Kiwelu
Mhe. Capt. John Damian Komba
Mhe. Celina Ompeshi Kombani
Mhe. Anna Maulidah Komu
Mhe. Suleiman Omar Kumchaya
Mhe. William Jonathan Kusila
Mhe. Omar Shabani Kwaangw'
Mhe. Michael Lekule Laizer
Mhe. James Daudi Lembeli
Mhe. Castor Raphael Ligallama
Mhe. Devota Mkuwa Likokola
Mhe. Dr. Festus Bulugu Limbu
Mhe. Benedict Kiroya Losurutia
Mhe. Sameer Ismail Lotto
Mhe. Edward Ngoyayi Lowassa
Mhe. George Malima Lubeleje
Mhe. Joelson Mpina Luhaga
Mhe. William Vangimembe Lukuvi
Mhe. Anna Richard Lupembe
Mhe. John Paul Lwanji
Mhe. Clemence Beatus Lyamba
Mhe. Susan Anselm Jerome Lyimo
Mhe. Ernest Gakeya Mabina
Mhe. Joyce Luhamanilo Machimu
Mhe. Ephraim Nehemia Madeje
Mhe. Prof. Jumanne Abdallah Maghembe
Mhe. Fatma Mussa Maghimbi
Mhe. John Pombe Joseph Magufuli
Mhe. Dr. Milton Makongoro Mahanga
Mhe. Dr. Binilith Stano Mahenge
Mhe. Mwantumu Bakari Mahiza
Mhe. Ezekiel Magolyo Maige

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hauruhusu kuendelea na shughuli zetu za Bunge kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.43 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 29 Desemba, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*